JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

April, 2026

Dodoma

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OWM TAMISEMI

Namba za simu:
Mkuu wa Shule: 0756756061 / 0689522984
Makamu Mkuu wa Shule: 0783214454

NYANUNGU SEKONDARI
S.L.P 345,
TARIME
……………….

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ........................................................................................
S.L.P.................................

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYANUNGU ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME, MKOA WA MARA MWAKA…………………………..**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …………….. na atasoma tahasusi ya .........................

Shule ya Sekondari Nyanungu ipo umbali wa Km 16 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Tarime (Nyamwaga) na takribani Km 41 kutoka mji mkuu wa wilaya ya Tarime. Usafiri kutoka Tarime mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Rebu sokoni Tarime Mjini. Nauli ni Shilingi 7,000/- kwa magari ya abiria na kwa pikipiki ni Shilingi 20,000/-.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ..................... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ....................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………………..

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni Suruali mbili kwa Wavulana nyeusi Maelezo ya mshono; suruali zenye marinda mawili,zisiwe za kuvalia kwenye makalio kwa staili ya kata "K" wala zisizo buruza chini kwa staili ya "Pito" na zisiwe Modo, chini ziwe size 18 na iwe na pindo (turn up).
ii. Mashati meupe mawili yenye mikono mirefu;
iii. Sare ya Michezo ni track suit moja Blue yenye nembo ya shule (inapatikana shuleni).
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule; vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta rangi ya kijani kibichi shingo ya V na nembo ya shule (zinapatikana shuleni).
viii. Tai rangi nyeusi.
ix. Tisheti (T-shirt) rangi ya blue yenye nembo ya Shule na (zinapatikana shuleni).

NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani shuleni isipokuwa nguo za shule tu.

x. Suruali mbili za kushindia rangi damu ya mzee.

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 10 (Counter books);
ii. Ream (A4) ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Scientific Calculator;
v. Godoro liwe na vipimo vya futi 2.5 kwa 6 (super banco)
vi. Mashuka Jozi 2; jozi moja blue na moja pinki, blanket moja, mto na foronya, pia aje na chandarua moja rangi ya blue.
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Ndala za kuogea
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 (moja lita 10 moja lita 20) zenye mifuniko;
xi. Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake.

xii. Vifaa vya usafi;

| Tahasusi ya HGK walete | Tahasusi ya HGL walete |
|---|---|
| Kwanja 1 | - Reki 1 |
| Jembe moja na mpini | - Jembe moja na mpini |
| Mfagio laini 1, mopa 1 | - Mfagio mgumu 1, |
| Dawa ya chooni lita 5 (nzito) | - Dawa ya chooni lita 5 (nzito) |
| | - Mopa 1 |

### 2.3 **Michango mbalimbali**

Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

NB: Michango yote ilipwe kupitia akaunti ya shule NMB 30401000055 yenye jina Nyanungu Secondary School

NB: Mzazi unashauriwa kumkatia mtoto bima ya afya na aje nayo pindi anaporipoti shuleni.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;

MUHIMU:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara; ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;

xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu
   i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
   ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
   iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
   iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule ...............

Jina la Mkuu wa Shule: CASMIRY EMMANUEL KANGA

Mhuri wa Mkuu wa Shule .............

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule: 0756756061 / 0689522984
- Makamu Mkuu wa Shule: 0783214454

Kiambatanisho i

FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA (MEDICAL EXAMINATION FORM).

Full name ....................................................Age .......... Height (in cms) ......... Weight (in kgs) ......

1. Blood count ....................……………(Red and White) ...........……………
2. Stool Examination ........................................................................................
3. Urine Analysis ...............................................................................................
4. Syphilis and other V.D ......................................................................................
5. T.B and Leprosy Test .........................................................................................
6. Eye Test .....................................................................................................................
7. Ear Test ..............................,,,,,.…………………………………………………………...
8. Chest test ...................................................................................................................
9. Abdominal Test .........................................................................................
10. Blood Group (very crucial) .........................................................................
11. Spleen ................................. ……………………………………………………
12. H.I.V Test, Positive .................... Negative ....................... (Tick where necessary)

Additional information e.g Physical defects or impairments infection chronic or family Diseases (eg Sickle cell). .........................................................................................

I certify that the above student is fit/pursues Secondary Education

Name …………………………………… Signature ........................................................

Designation ...............................................................

Station .........................................................................

Date ...................................................

Kiambatanisho ii

a) HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI.

1. Jina la kwanza ...................................... Jina la kati .......................................
   Jina la mwisho ...........................................
2. Jina la Mzazi/Mlezi ...................................................
3. Kama ni Mlezi: uhusiano ..........................................
4. Namba za simu za Mzazi/ Mlezi ...............................
5. Anwani ya kudumu ya Mzazi/Mlezi ............................
6. Mahali mwanafunzi alipozaliwa: Kijiji cha ................. Kata ya .............. Wilaya ..........
   Mkoa ............................
7. Dini .................................. Dhehebu .............................
8. Unaingia kidato cha ........................ Tarehe/Mwaka ..........................
9. Kutoka shule ya Msingi/Sekondari ............................... Wilaya .............. Mkoa .............
10. Kazi anayofanya Mzazi/Mlezi wako ni ...................... Mahali ............................
11. Usafiri kutoka hapa shuleni hadi nyumbani kwenu ni: (Toa maelezo)
    - ................................
    - ................................
12. Ndugu wengine ambao wanaweza kupelekewa habari muhimu juu yako au masuala ya shuleni ni:-

| Jina la ndugu | Uhusiano | Namba za simu |
|---|---|---|
| i) | | |
| ii) | | |
| iii) | | |

13. Unalipiwa/utalipiwa michango na: Taja jina na anwani yake, au namba za simu .....................................
14. Taarifa za wazazi: A. Wapo ☐ B. Wamefariki ☐ (weka vema ( √ ) panapohusika)
15. Kabla hujaja hapa shuleni umepimwa na daktari? ndiyo/hapana. ni ugonjwa upi ni wakudumu kwako? ………………………………………
16. Sifa maalumu kama unazo …………………………………………………...
17. Nakiri kuwa maelezo niliyotoa hapo juu ni sahihi.
    Saini ya Mzazi/Mlezi …………………….. Saini ya Mwanafunzi ………………………….

b) MKATABA WA MWANAFUNZI WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi (jina la mwanafunzi) ............................................................... nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na shule hii. Naahidi kufuata sheria za shule na taratibu zote kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule. Pia naahidi kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa yoyote ya jinai niwapo shuleni hapo.

Jina la Mwanafunzi .........................................................

Saini ya Mwanafunzi .......................................... Tarehe ............................

Kiambatanisho iii

## FOMU YA MZAZI/ MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE

Mimi (Jina la mzazi/mlezi)..................................................................... Ambaye ni Mzazi/Mlezi wa (Jina la mwanafunzi) ....................................................... nimeyasoma na nimekubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ya Sekondari Nyanungu ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule. Pia naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadae awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

Aidha naahidi kuwa nitamlipia na kumpatia mwanangu huduma muhimu za shule kama vile; Michango ya shule, Sare za shule na michezo; Matibabu; Vifaa vya kujifunzia ikiwa ni pamoja na madaftari, kalamu, vitabu n.k

Jina la Mzazi/Mlezi ...............................................Namba ya simu ..............................................

Kitongoji.................................................... Mtaa/Kijiji .........................................................

Anuani: S.L. P ................................ Wilaya .......................................................

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ........................................... Tarehe .................................